

# Pambazuko *Ukweli Hauna Kutu*

Toleo Namba 010

Jumatatu Septemba 12-18, 2022

**Hasira za serikali zionekane kwa mafisadi Uk. 2**

**Basi,  
asikilizwe  
Jaji Chande  
Uk. 5**



**Rais Samia  
amtaja Mungu  
mara nane**

● *Aliomba Kanisa Katoliki kusaidia  
kutokomeza mfumo dume*

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye  
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

### Hasira zionekane kwa mafisadi

**M**ARA kadhaa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Majaliwa Kassim Majaliwa, amesikika akifoka, akionekana kukerwa na zaidi sana akithibitika kukasirika kwa matukio anayoyataja kuwa ni ubadhirifu na matumizi mabaya ya ama madaraka au fedha za walipakodi anapokuwa katika ziara za kukagua miradi ya maendeleo.

Wiki iliyopita - Septemba 8, Waziri Mkuu Majaliwa akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Tabora, alifika kwenye mradi wa ujenzi wa Chuo cha Veta Uyui, ambako alishangazwa kusikia kuwa kibanda cha mlinzi wa chuo hicho kimegharimu Sh. milioni 11.

Waziri mkuu alisema kwa muonekano, kibanda kile hakiwezi kuchukua kiasi hicho cha fedha alichoelezwa na kwamba huenda kuna ubadhirifu umefanywa na kuamuru Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (Takukuru) kuwakamata na kuanza kuwachunguza wote waliohusika katika mchakato wa ujenzi huo.

Hilo ni tukio la hivi karibuni ambalo limemuonyesha, kwa mara nyingine, kiongozi mkuu wa shughuli za serikali bungeni na mshauri -mtendaji wa karibu kabisa wa Rais Samia Suluhu Hassan, akifoka na kuamuru watendaji kukamatwa akiwa kwenye kadamnasi.

Pamoja na kwamba ni hatua nzuri kwa kiongozi wa juu kuonekana kukwera na yanayoendelea katika utekelezaji wa majukumu ya kuhakikisha maendeleo yanapatikana, bila kuwaibia wananchi kodi zao,

bado kuna maeneo ambako Waziri Mkuu na uongozi mzima wa serikali, wameshindwa kuonyesha hasira zao.

Maeneo hayo ni yale yanayothibitika katika vitabu vya Mkguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwamba kuna wizi mkubwa wa fedha za walipakodi wa Tanzania na hata wale wanaoleta fedha kwa njia ya mikopo na hata misaada kutoka nchi washirika wa maendeleo.

Kila mwaka CAG amekuwa akiibua madudu ya kutisha katika halmashauri, taasisi, wakala, kampuni na hata mashirika yanayoendeshwa na serikali moja kwa moja au kuwa na ubia, lakini hasira na sauti za kufoka hazisikiki kuwa kuu na zenye ukali kwa wahusika wanaoweza kuwekwa kwenye kundi la 'mapapa wezi.'

Pamoja na ubaya wa ubadhirifu mdogo, madhara yake yanaweza kuwa makubwa ikiwa yatajikusanya hata kufikia viwango vya ufisadi, ambao una ubaya mkubwa zaidi na kuwa na madhara yanayoumiza jamii pana zaidi.

Watanania wanapenda kuona serikali ikichukua hatua kali zaidi kwa wote wanaofisidi nchi hii, hasa hao wanaobainika kukwapua fedha za maendeleo kwa manufaa binafsi, huku wakifanya mnyororo wa umasikini kuendelea kuwafunga wengi zaidi - na hata kupokewa na vizazi na vizazi.

Ikiwa hasira za serikali zitabaki kwa "vidagaa" tu, na mafisadi papa kuachwa, basi hata uchunguzi wa CAG na ushauri wake, hautakuwa na maana zaidi ya kujaza karatasi katika kabati za ofisi za wakubwa.



## Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: [pambazuko1@protonmail.com](mailto:pambazuko1@protonmail.com) ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## NUKUU



*“Siasa Hazikuja kwa lengo la Kuleta Uhasama bali kukuzwa demokrasia katika nchi” - Rais Mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassani Mwinyi katika mahojiano maalumu na TBC 2016 kwenye maadhimisho ya miaka 55 ya Uhuru wa Tanzania*



1926 – 2022



Malkia Elizabeth II wa Uingereza amefariki dunia Alhamisi iliyopita - Septemba 8, 2022 akiwa na miaka 96 baada ya kutumikia dhamana hiyo kwa miaka 70. Malkia, ambaye jina lake halisi ni Elizabeth Alex-andra Mary Windsor, atakumbukwa kwa kusimamia kusambaratika kwa himaya kubwa ya koloni la nchi yake na kupatikana kwa uhuru kwa nchi nyingi za Afrika. Malkia au Mfalme wa Uingereza ndiye Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Madola na Gavana Mkuu wa Kansia la Anglikana. Baada ya kifo chake, Uingereza itaongozwa na kijana wake mkubwa, ambaye sasa atajulikana kuwa ni Mfalme Charles III. (Picha: Jeff J. Mitchell / Getty Images).

## Basi, asikilizwe Jaji Chande

Na Dkt. Bullet RUHINDA

**W**ASOMAJI wa Kitabu Kitakatifu cha Wakristo, Biblia, watakuwa wamekutana na aya isemayo, “je jambo jema laweza (ku)toka Samaria?”

Katika Uyahudi ya zamani, Kijiji cha Samaria kilidharaulika zaidi, watu wake walionekana wenye hadhi ya chini, wasiokuwa na werevu wowote, hivyo haikutegemewa wawe chanzo cha kitu chochote katika nchi.

Hata hivyo, siyo kweli kwamba Wasamaria walikuwa wajinga au wapumbavu, bali kuna wananchi wenzao waliamua kuwaona watu wasiokuwa na maana.

Katika jamii nyingi hata za ‘kisasa,’ kuna watu au kikundi cha watu ambao hudhani wao ndio wanaweza kuwa na mawazo mazuri kuliko wenzao. Na endapo hao wanaodharauliwa, hata wakija na hoja nzuri, hubezwa.

Wimbo wa Katiba mpya umeanza miaka mingi. Wapinzani (sipendi kuwaita hivyo, bali watu wa mrengo tofauti) wamekuwa mstari wa mbele kupigania mabadiliko ya Katiba kwa madai kwamba Katiba ya sasa haina majibu kwa maswali ya sasa.

Watawala na hasa chama tawala, Chama Cha Mapinduxi (CCM) wamekuwa mbele kupinga kupatiana kwa Katiba mpya hata kama wao wanaona au wanakubaliana na hoja za wapinzani kwamba Katiba ya sasa haina majibu ya maswali ya sasa.

Lakini watawala hao wamekuwa wakisema; “je, jambo jema laweza kutoka Samaria?” Kwenye neno Samaria, soma “kwa wapinzani.”

Baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kukutana na “Wasamaria” alikuja na hoja ya kuunda kikosi kazi cha kuangalia mchakato wa Katiba. Ghafila, wale walioona wenzao ni “Wasamaria,” nao wakaanza “kuona” umuhimu wa Katiba mpya. Ikawa kwamba zile hoja za



Jaji Chande

kutaka “maendeleo kwanza” ni kama zimepumzishwa kwa muda.

Hoja ya Katiba imekuwa sasa nzuri baada ya tamko la mtu ambaye siyo Msamaria! Gazeti moja la kila siku Septemba 8, 2022 limemnukuu Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Chande Othman akisema; “tusiwe na hofu kubadili Katiba” - akitoa faida ambazo Kenya wanazipata kwa kuwa na katiba nzuri.

Lakini, Jaji Chande siyo Mtanzania wa kwanza kuonesha uzuri wa Katiba ya Kenya na yapi Tanzania inaweza kuiga kutokana na Katiba hiyo.

Ni matumaini ya wengi kwamba Jaji Chande atasikilizwa na wahusika na maoni yake kuchukuliwa kwa uzito mkubwa kwa sababu siyo “Msamaria.”

Ikiwa maoni na mtazamo huu wa Jaji Chande ambao ameuweka wazi, utakubalika, basi tutambue kuwa kuna mengi ambayo “Wasamaria” wamependekeza, lakini yamedharauriwa kwa kuwa tu wanatoka Samaria.

**Tutafakari.**

### Zuma alalama kufilisika

**A**LIYEKUWA Rais wa Afrika Kusini, Jacob Zuma anaelezwa kutetereka kifedha kiasi cha kuanza kuomba michango kutoka kwa mashabiki, ndugu na jamaa ili kulipa madeni.

Zuma ambaye alikuwa kiongozi wa nchi hiyo kwa miaka tisa (2009-2018) na makamu wa rais kwa miaka sita (1999-2005), licha ya kupewa pensheni ya Sh. milioni 32, bado anadai kuwa na ukata unaokwamisha maisha yake ya kawaida.

Akiwa anakabiliwa na kesi nyingi za ufisadi na kuendelea kulipa fedha za serikali alizobainika kutumia kujenga kasri kijijini kwake Nkandla, pia anadaiwa na benki ya VBS kiasi cha Sh. milioni 870 alizokopa. Benki hiyo ilifilisika na sasa iko chini ya uangalizi wa benki kuu ya nchi hiyo.

Kupitia wakfu wake, Zuma amekuwa akitembeza bakuli kwa watu na taasisi mbalimbali akiomba msaada wa fedha ili kukabili madeni makubwa anayodai “yamemtoa kwenye mstari wa maisha.”

Zuma mwenye miaka 80, wake watano na watoto 24, yuko katika uangalizi wa mahakama, baada ya kupewa ruhusa ya kukaa nyumbani kufuatia kifungo chake cha miezi 15 baada ya kukutwa na hatia ya kudharau Tume ya Uchunguzi iliyomuita ili kumhoji na kukaidi.

*Johannesburg (DM)*

### Mchina agombea ubunge Lesotho

**M**GOMBEA ubunge Jimbo la Basotho, nchini Lesotho, Jason Shao ameahidi “makubwa” kwa wapiga kura wake endapo atashinda katika uchaguzi uliopangwa kufanyika Oktoba 7, mwaka huu.

Shao ambaye ni raia wa nchi hiyo baada ya kuandikishwa mwaka 2006 – akitokea China, ni mfanyabiashara mkubwa wa eneo hilo na mji mkuu wa Maseru.

Anaahidi kuwa mara baada ya

kutangazwa mshindi wa kiti cha ubunge, kazi kubwa atakayofanya ni kuhakikisha anahimiza uwekezaji mkubwa wa viwanda ili vijana wa jimbo lake na maeneo mengine ya nchi hiyo, kupata ajira.

Shao anasema pia atashawishi kubadilishwa kwa mfumo wa elimu ili iendane na kasi ya kukua kwa sanyansi na teknolojia, hasa kuhimiza elimu-vitendo na siyo nadharia pekee.

*Basotho (MaseruMetro)*



*Jason Shao*

### Polio hatari New York

**Y**AWEZA kudhaniwa hadithi, lakini ndiyo ukweli wenyewe kwamba jiji kubwa, lenye utajiri wa kutosha na uhakika wa hali ya usalama wa afya, sasa limewekwa karantini.

Gavana wa Jiji la New York, Marekani, Kathy Hochul - Ijamaa iliyopita alitangaza hali ya hatari kwa wakazi wa jiji hilo akitahadharisha kuenea kwa kasi kwa kuwepo mlipuko wa ugonjwa wa polio.

Hochul, gavana wa 57 na kuwa wa kwanza mwanamke, alitangaza hali hiyo ikiwa ni jitihada za kuwanusuru wahudumu wa afya ambao wamekuwa wakikutana na wagonjwa wengi kiasi cha kuhatarisha uhai wao.

*New York (NYT)*

## Kibarua kwa Ruto kugawa 'keki'

Na Wanderi KAMAU

**K**ESHO Rais Mteule wa Kenya, Dkt. William Ruto ataapishwa na kuanza kazi rasmi ya kuongoza taifa hilo.

Moja ya kazi ngumu kwake ni kutimiza ahadi alizotoa kwa washirika wake wa kisiasa, huku idadi kubwa ya wanasiasa wanaoendelea kuhamia katika chama chake Kenya Kwanza wakiongezeka.

Kwenye kampeni zake, Dkt. Ruto aliahidi "kutowaacha nje" wanasiasa waliohangaishwa na serikali iliyokuwa madarakani ikiongozwa na Rais Uhuru Kenyatta, kwa "kuamua kuwa marafiki zake."

"Tutabuni serikali kubwa itakayokuwa na nafasi kwa kila mmoja. Itakuwa nyumba kubwa ambayo itatoa nafasi kwa kila mmoja wetu," anasema Dkt. Ruto.

Hata hivyo, ongezeko la wanasiasa wanaoendelea kujiunga na mrengo huo limeibua wasiwasi miongoni mwa washirika wake, baadhi wakisisitiza kuwa hawatakuwabi watu waliojiunga dakika za mwisho mwisho "kugawiwa keki yao."

Hadi sasa, baadhi ya vigogo wa kisiasa ambao wamejiunga na kambi ya Dkt. Ruto ni magavana wa zamani Kiraitu Murungi (Meru), James Ongwae (Kisii), mbunge David Ochieng (Ugenya), seneta mpya wa Mandera Ali Roba, miongoni mwa wengine.

Hata hivyo, tayari, baadhi ya washirika wake wamejitokeza kulalamikia idadi kubwa ya "wageni" wanaohamia kambi hiyo, akiwamo mbunge Sylvanus Osoro (Mugirango Kusini), anayesisitiza kuwa kabla ya wanasiasa hao kuhamia Kenya Kwanza, Dkt. Ruto tayari ana mikataba ya kisiasa na wale alikuwa nao kabla.

"Tunawakaribisha wageni. Hata hivyo, lazima wafahamu kuwa wanaingia katika nyumba yenye wenyeji. Hivyo, lazima wafahamu kuwa hakuna mgao wowote wa mamlaka watakaopata," anasema Osoro.

Aliyekuwa mbunge wa Gatundu Kusini, Moses Kuria, pia ametoa kauli kama hiyo,



William Ruto

akisema wale wanaotegemea kupata mgao wa serikali kwa kujiunga na Dkt. Ruto "wamechelewa sana."

Kulingana na wadadisi wa siasa, huenda mwelekeo huo ukaendelea kushuhudiwa katika siku chache zijazo, ikizingatiwa kuwa Dkt. Ruto bado hajafanya teuzi muhimu kama uteuzi wa baraza la mawaziri, manaibu wao na wakuu wa mashirika tofauti ya serikali.

"Kibarua alichonacho Dkt. Ruto ni kuwapa nafasi serikalini washirika wake ambao wamekuwa naye kwa muda mrefu na kuwakaribisha wanasiasa wabaya wanaohama kutoka vyama vingine au wale waliohinda nafasi mbalimbali kupitia ugombea binafasi.

Hata hivyo, wadadisi wanaonya kuwa huenda Dkt. Ruto akaanza kuwakasirisha baadhi ya washirika wake alioingia nao mkataba kutoka maeneo yaliyompigia kura kwa wingi kwenye uchaguzi wa Agosti 9, 2022.

Makala haya yalichapishwa kwa mara ya kwanza na gazeti la Taifa Leo. Yamehaririwa kidogo kuendana na nafasi na staili ya Pambazuko.



### Siasa safi: Uundaji wa taifa

Na Dkt. Askofu Stephen MUNGA

**T**UNAPOZUNGUMZIA siasa, ama nzuri au mbaya, lazima kwanza liwepo taifa (state). Neno taifa hapa linatumiwa kumaanisha jumua iliyoundwa kama jamii ya kisiasa chini ya serikali moja.

Tunapozungumzia siasa safi tunamaanisha taifa lililoundwa kwa mfumo wa kanuni (rules) ambamo umejengwa uwiano wa matarajio ya watu kwa misingi ya heshima ya utu. Mfumo huu wa kanuni huchukua taswira ya jamii, tofauti na mkusanyiko wa mtu binafsi mmoja mmoja.

Jamii ina umoja na uwiano wa matarajio kuliko kila mtu peke yake na kila mmoja na lwake. Mtazamo huo wa jamii hufunua uwepo wa taifa. Tangu uelewa huo wa taifa ndipo twaweza kuzungumzia ujenzi wa siasa safi.

Hivyo, siasa safi ni matokeo ya usafi wa mtandao wa kanuni zinazozingatia uwiano wa matarajio ya watu katika usahihi na uhalisia wake. Hapa ni kama tunarejeshwa katika nadharia ile tuliyotaja katika makala yaliyopita juu ya ‘nafasi ya asili’ (original position).

Taifa lililoundwa kwa mfumo wa kanuni ambamo imezingatiwa uwiano wa matarajio kwa kuzingatia heshima ya utu ni taifa la watu huru. Katika mifumo ya kidemokrasia mfumo huo wa kanuni husimama katika mihimili mitatu ya serikali – Bunge, Mahakama na Utawala.

Taifa kwa maana niliyoitoa hapo juu huegemea zaidi katika namna ya utendaji wa mihimili hiyo. Ni muhimu na ni lazima katika uundaji wa siasa safi watu katika taifa waone uwepo wao na kujiona kuwa sehemu katika uundwaji na utekelezwaji wa mfumo huo wa kanuni.

Pia niongeze kwamba ni dai la msingi kuwa kila mtu aone uwepo wa wengine ni muhimu kama ilivyo kwa haki na wajibu wao katika mfumo huo wa kanuni.

Hii ndio sababu uelewa wa taifa nimeusimamisha katika msingi wa



Mwl. Nyerere- Muumini mkubwa wa siasa safi

jamii na wala sio katika mtu peke yake binafsi na kila mtu na lwake. Mtu niliyemtengeneza katika gurudumu la watu ni yule ambaye uwepo wake na uwajibikaji wake huthibitika kwa uwepo wa wengine. Kila mtu yupo kwa sababu wengine wapo.

Mfumo huo wa kanuni ndio unaotoa picha ya siasa nzuri au siasa mbaya. Hapa ndipo inafaa turejee tena sehemu ile tuliyotengeneza mtu katika gurudumu la kwanza la “watu.” Moja ya fikra nilizoibua katika kumtengeneza mtu yule ni ile kwamba mtu huyo ni mshiriki wa umbaji wa fikra za siasa.

Hivyo twaweza kusema watu ndio waumbaji wa mifumo hiyo ya kanuni. Je, ni watu gani taifa linao wa kutengeneza mifumo ya kanuni? Je, hao ni jamii ya wenye dhamira ya dhati ya kutengeneza mifumo inayozingatia uwiano wa matarajio katika mwanga wa heshima ya utu?





Na Evarist Chahali  
evarist@chahali.com

## Mapokeo kinzani kifo cha Malkia

**A**LHAMISI iliyopita, Uingereza alilikumbwa na msiba mkubwa, kufuatia kufariki dunia kwa Malkia Elizabeth wa Pili. Malkia huyo alifikwa na umaui baada ya kudhoofika kwa afya yake kwa muda mfupi. Kifo hicho kilitokea kwenye makazi yake aliyoyapenda zaidi yaliyoko Uskochi.

Hadi anafariki dunia akiwa na umri wa miaka 96, Malkia Elizabeth wa Pili alikuwa madarakani kwa miaka 70 na siku 127, muda ambao ni rekodi katika utawala wa Ufalme wa Muungano wa Britania na Eire ya Kaskazini (kwa Kiingereza, the United Kingdom of Great Britain and Northern Ireland).

Muungano huo ni wa mataifa manne – Uingereza (England), Uskochi (Scotland), Welisi (Wales) na Eire ya Kaskazini (Northern Ireland).

Kifo cha malkia huyo ambacho kimewezesha kutangazwa kwa mwanawe wa kwanza, Charles kuwa mfalme anayetambulika rasmi kuwa Charles wa Tatu, kimepokelewa kwa majonzi makubwa miongoni mwa Waingereza wengi na watu wa sehemu mbalimbali duniani.

Kwa mujibu wa ratiba, malkia huyo atazikwa tarehe 19 ya mwezi huu, ambapo kwa sasa nchi ipo kwenye maombolezo ya siku 10. Kadhalika nchi mbalimbali duniani zimetangaza kupeperusha bendera nusu mlingoti kumuenzi mtawala huyo ambaye pia alikuwa mkuu wa Jumuiya ya Madola.

Kuna mambo muhimu mawili kuhusiana na kifo hicho; kwanza, kwa hapa Uingereza, japo idadi kubwa ya watu wamekipokea kwa uchungu, wakazi kadhaa wa Uskochi na Eire ya Kaskazini “wamefurahia” kutokana na mataifa hayo mawili, pamoja na Welisi, kuwa “makoloni” ya Uingereza (England) huko nyuma.



Malkia Elizabeth wa Pili

Na hadi wakati huu, kuna upinzani wa kutosha tu dhidi ya “muungano” uliopo. Mwaka 2014, Uskochi ilipiga kura ya maoni kuhusu uhuru wake, na japo waliotaka taifa hilo libaki kwenye muungano walishinda, kuna jitihada za kufanya marudio ya kura hiyo.

Pili, angalau kwenye mitandao ya kijamii, kumekuwa na malalamiko mengi dhidi ya utawala wa Malkia Elizabeth wa Pili, kwani ndio ulioshiriki kikamilifu kwenye uovu wa ukoloni wa sehemu mbalimbali duniani, hususan barani Afrika.

Malalamiko zaidi ni kwamba hadi anafariki, Malkia huyo hakuwahi kuomba msamaha kwa maovu yaliyofanywa na utawala wake.

Hili la pili limenikumbusha kuhusu “vilio vya chinichini” vinavyoendelea nchini Tanzania miongoni mwa wahanga wa utawala uliopita ambao hadi sasa “hawajaombwa radhi.” Nitaongelea kuhusu hili katika makala zijazo.

**Mwisho, kwaheri Malkia Elizabeti wa Pili**

### Rais Samia amtaja Mungu mara nane

Na Simon MKINA

**R**AIS Samia Suluhu Hassan amemtaja Mungu mara nane katika hotuba yake wakati akizungumza na Watanzania kupitia kwa maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania.

Huku akitaja namna Mungu “alivyoipendelea Tanzania” kwa neema yake rasilimali, pia aliwaomba maaskofu kusaidia kutokomeza mfumo dume nchini.

Rais Samia alisema serikali yake inahitaji msaada wa maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania kushirikiana na serikali anayoiongoza kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa mtazamo wake kutokomeza mfumo dume na mizizi yake nchini kabla ya mwaka 2072.

“Nina imani kwamba, katika miaka mingine 50 inayokuja, chini ya uongozi wa Kanisa, na kwa kushirikiana na serikali, tutakuwa tumetoka kwenye dhana ya kutaka usawa wa kijinsia kiasi kwamba jambo la kuwa na viongozi wanawake, hata katika ngazi ya urais litakuwa la kawaida sana,” alisema Rais Samia.

Samia aliyatamka maneno haya jana, katika Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam, ambako alikuwa mgeni rasmi kwenye Jubilee ya Miaka 50 ya kuanzishwa kwa Chama cha Kitume cha Wanawake Wakatoliki Tanzania (Wawata)

Kauli ya Rais Samia ilitamkwa mbele ya Maaskofu Katoliki wakiongozwa na Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Gervase Nyaisonga.

Gazeti la Pambazuko linafahamu kwamba, Rais Samia alianza kupiga vita mfumo dume tangu alipoingia madarakani mwezi Machi mwaka 2021.

Machi 23, 2021, akiwa kwenye mazishi ya kitaifa ya Rais Magufuli, Rais Samia alisema; “aliyesimama mbele yenu, ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye maumbile yake ni mwanamke. Hivyo, kwa wale ambao bado wana mashaka, nataka kuwahakikishia

kwamba, maumbile yangu ya kike hayatakuwa kikwazo cha dhamira yangu ya kukidhi matakwa ya uongozi ubora.”

Mwezi mmoja baadaye, Aprili 22, akiwa anahutubia Bunge mjini Dodoma, Rais Samia alisema maneno yafuatayo:

“Mimi ni Rais wa kwanza mwanamke. Wakati mwingine utendaji wangu umekosolewa mara kadhaa kwa sababu tu ya maumbile yangu kama binadamu mwanamke. Lakini, kwa mujibu wa kanuni za maumbile, ninafahamu kuwa, Muumba wetu hakuumba akili dhaifu kwa ajili ya mwanamke na akili bora kwa ajili ya mwanamume.”

Kauli hizi kutoka kwa mkuu wa nchi ziliashiria kwamba, moja ya changamoto alizokumbana nazo akiwa kiongozi wa nchi ni kero ya kuwepo dhana ya mfumo dume.

Ni katika muktadha huu wa kihistoria, Rais Samia anasema kuwa ndoto yake ni kwamba, “katika miaka mingine 50 inayokuja,” kama taifa, “tutakuwa tumetoka kwenye dhana ya kutaka usawa wa kijinsia.”

Kwa mujibu wa kitabu cha Steven Goldberg, kiitwacho “The Inevitability of Patriarchy,” kama kilivyochapishwa mwaka 1973, huko New York, Marekani, na kampuni ya “William Morrow,” tunaambiwa kwamba:

“Mfumo dume ni mfumo wa kisiasa, kiuchumi, kidini au kijamii ambao unafungamanisha mamlaka ya uongozi na maumbile ya kiume zaidi kiasi kwamba nafasi nyingi za uongozi hujazwa na wanaume.” (uk. 30).

Goldberg anafafanua uwepo wa mfumo dume katika sehemu nyingi duniani kwa kutumia nadharia ya “ukuu wa maumbile dhidi ya mapokeo,” yaani, “the dominance of nature over nurture theory.”

Kwa mujibu wa nadharia hii, wanaume siku zote wataongoza wanawake kwa sababu ya hoja ifuatayo; mosi, anadai kwamba, jamii zenye kukumbatia usawa wa kijinsia, ambazo ni kinyume cha jamii zenye kuongozwa na itikadi ya mfumo

## Rais Samia amtaja Mungu mara nane

dume, hazipo mahali popote duniani.

Pili, anaeleza kwamba, nguvu zinazoongoza uhusiano kati ya wanawake na wanaume, siyo nguvu za kimapokeo, bali ni nguvu za maumbile ya kibayolojia.

Hivyo, Goldberg anahitimisha kwamba, kwa sehemu kubwa, mfumo dume ni itikadi isiyopukiki kwa sababu ya tofauti za kimaumbile kati ya wanawake na wanaume.

Hata hivyo, nadharia ya Goldberg kuhusu “ukuu wa maumbile dhidi ya mapokeo” inakosolewa na Rais Samia anaposema kuwa, “Muumba wetu hakuumba akili dhaifu kwa ajili ya mwanamke na akili bora kwa ajili ya mwanamume.”

Hivyo, Rais Samia hapingi madai kwamba, kuna tofauti za kimaumbile na kitabia katika ya wanaume na wanawake; anakubali kwamba, wanaume na wanawake wanatofautiana katika anatomia, fiziolojia, saikolojia na hisia.

Anachopinga ni kwamba, katika jamii inayoongozwa na mfumo dume, usawa kati ya wanawake na wanaume unatweza kupita kiasi, wakati tofauti kati yao zinakwezwa kupita kiasi kwa ajili ya kuwanufaisha wanaume na kuwakandamiza wanawake.

Na ukweli ni kwamba, usawa kati ya wanawake na wanaume wenye kuhalalisha wanawake kufanya kazi nyingi zinazofanywa na wanaume upo wa kutosha. Hata Katiba ya Tanzania (1977) inasisitiza habari ya usawa wa binadamu.

Kwa ujumla, kuna usawa na utofauti kati ya wanawake na wanaume katika ngazi ya anatomia, fiziolojia, siasa, falsafa, na ngazi ya teolojia. Tuanze na ufafano na usawa kati yao.

Kianatomia na kifiziolojia, usawa kati ya wanaume na wanawake upo katika maeneo yapatayo 15.

Kwa mfano, wote wana mfumo wa kupumua, mfumo wa chakula, mfumo wa damu, mfumo wa kutoa uchafu mwilini, mfumo wa kucha na nywele, mfumo wa mifupa, mfumo wa homoni, mfumo wa tezi, mfumo wa kinga za mwili, mfumo

wa neva, mfumo wa milango mitano ya fahamu, mfumo wa misuli, mfumo wa uzazi, na mfumo wa kromozomu 45 zinazofanana na kromozomu moja ya uzazi iliyo tofauti.

Kisiasa na kifalsafa, wanawake na wanaume ni sawa mbele ya Katiba ya Tanzania (1977), kwani, katika ibara ya 12(1), inatamkwa kwamba binadamu wote ni sawa. Usawa huo upo kwenye akili na utashi.

Kifalsafa, wanawake na wanaume wanao uwezo wa kuteua malengo, kuchagua mbinu za kufanikisha malengo hayo, na kutekeleza mbinu hizo hadi kufanikisha malengo husika.

Kwa sababu hii, Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, kupitia Azimio la Dar es Salaam, mwaka 1978, alitamka kwamba, “Uwezo wa binadamu kufanya matendo yanayoongozwa na kumbukumbu na akili, kwa ajili ya kufanikisha malengo aliyojiweka, ndio unamtofautisha na wanyama wengine.”

Na kiteolojia, tunaambiwa kwamba, akili na utashi ndio sifa kuu mbili zinazowafanya wanawadamu watambuliwe kama viumbe ambao ni “mfano wa Mungu.”

Tunasoma hayo kwenye Biblia ndani ya Kitabu cha Mwanzo (2:26), kwenye Biblia ndani ya Kitabu za Zaburi (8:4) na kwenye Kurani ndani ya kitabu cha Sura Baqarah (115).

Mwanasaikolojia anayeishi Dar es Salaam, Suleiman Hamduni anaeleza kuwa zipo tafiti za kisayansi zinazothibitisha mtazamo wa Rais Samia kwamba, hakuna tofauti ya maana katika namna akili za wanawake na wanaume zinavyofanya kazi.

“Kwa sababu ya ushahidi huu, ajenda ya Rais Samia kutokomeza mfumo dume Tanzania, ni wazo la kuungwa mkono kwa nguvu zote,” anaongeza mwanazuni huyo ambaye anaeleza aliwahi kuwa mhadhiri Chuo cha Ustawi wa Jamii, kilichopo Kijitonyama, Dar es Salaam.

### Uraia Pacha dhidi ya Hadhi Maalum

Na Godwin CHILEWA

**H**IVI karibuni Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alitangaza nia ya serikali kutunga sheria itakayowawezesha wanadiaspora kupewa Hadhi Maalum itakayolinda uzawa wao.

Katika maelezo yake aliyoyatoa akiwa safarini barani Ulaya na Marekani, Rais Samia alisema sheria hiyo (itakapopitishwa na Bunge), itamuwezesha Mtanzania aliyepewa uraia wa nchi nyingine kuwa na haki ya kuishi nchini Tanzania, kufanya kazi, kurithi na kumiliki mali na ardhi kwa mujibu wa sheria na taratibu zitakazowekwa.

Rais Samia hata hivyo, anasema sheria hiyo haitaruhusu uraia pacha jambo ambalo kwa miaka mingi wanadiaspora wamakuwa wakiliomba liwe.

Pengine kabla ya kusema lolote ni vyema ieleweke kuwa suala la uraia pacha siyo la wanadiaspora pekee, bali la Watanzania wengi, kwa manufaa ya Tanzania.

Kwa sababu hiyo, ni vyema kujua kama sheria ya Hadhi Maalum itakuwa na manufaa kwa taifa au la, na endapo inakuwa tofauti na sheria ya Uraia Pacha.

**Uraia Pacha:** Ni hali ya mtu kuwa na utaifa au uraia wa nchi mbili tofauti kwa wakati mmoja, kwa mujibu wa sheria za nchi husika. Mtu mwenye uraia wa nchi mbili anawajibika kutii sheria na kutimiza wajibu alionao katika nchi zote mbili kwa mujibu wa sheria ya kila nchi husika.

Wakati uraia wa nchi ya kwanza hupatikana kwa kuzaliwa, uraia wa nchi ya pili hupatikana kwa kuandikishwa katika nchi yenye sheria inayoruhusu uraia pacha. Hata hivyo, ili uweze kuwa na uraia pacha, ni lazima nchi ya uraia wako wa kwanza iwe ina sheria inayoruhusu uraia wa nchi mbili. Mfano wa nchi zinazoruhusu uraia pacha ni pamoja na Kanada, Italia, Australia, Irie, Uingereza, Kenya na nchi nyingine nyingi.



Rais Samia Suluhu Hassan

sheria itakayotungwa na Bunge la Tanzania ili kumruhusu mtu aliyepoteza uraia wa Tanzania kwa kupewa uraia wa nchi nyingine kuishi nchini Tanzania, kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo, na kumiliki mali/ardhi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopo sasa, sheria hii, itakapopitishwa, haitamrudishia muhusika baadhi ya haki za uraia alizopoteza kwa kuchukua uraia wa nchi ya kigeni, kwa mfano kupewa hati ya kusafirira. Mtu atakayepewa hadhi maalum atapaswa kulipia gharama za viza kila anapoingia nchini kama mgeni mwingine.

**Mwandishi aliwahi kuwa ofisa wa TISS kwa muda mrefu kabla ya kuhamia Marekani kwa shughuli zake za kanisa.**

Hadhi Maalum:Hadhi Maalum ni

---

## Tutakukumbuka Padre Ndakimubuza

**P**adre JohnBosco Ndakimubuza (64), wa Jimbo Katoliki la Rulenge-Ngara, alifariki tarehe 05 Septemba 2022, akiwa katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando, Mwanza.

Mauti yake imetokana na ugonjwa wa saratani uliopelekea figo zake na ini kushindwa kufanya kazi vizuri. Aliugua tangu Desemba 2021. Alipata matibabu katika hospitali Teule ya Biharamulo na baadaye katika Hospitali ya Rufaa Bugando, Mwanza.

Ndakimubuza alizaliwa tarehe tarehe 03 Februari 1959 katika kijiji cha Ruteme, Parokia ya Mabira Jimbo Katoliki la Kayanga Karagwe. Alimaliza elimu ya msingi katika shule ya msingi Nyakatuntu, Mabira (1973). Alihitimu elimu ya sekondari katika Seminari ya Katoke, Biharamulo (1977). Alimaliza masomo ya Falsafa katika Seminari Kuu ya Ntungamo, Bukoba (1979).

Alikamilisha masomo ya teolojia katika Seminari Kuu ya Kipalapala, Tabora, na kuhitimu (1984). Hatimaye alipata daraja la upadre mwaka 1984.

Kati ya 1984 na 2022, alipofariki, alikuwa amefanya kazi ya utume wa kipadre kama ifuatavyo: paroko msaidizi Parokia ya Nyamigere; mwalimu na mlezi katika seminari ya Katoke; Paroko katika parokia ya Nyaishozi; Mhasibu wa Jimbo la Rulenge-Ngara; paroko msaidizi parokiani Rwinyana; Paroko katika parokia ya Biharamulo; Dekano decania ya Biharamulo; meneja wa mashule ya jimbo; Katibu Mtendaji wa Idara ya ulinzi wa maisha ya binadamu; na hadi anakufa alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya seminari ya Katoke.

Marehemu Ndakimubuza atakumbukwa daima na wote aliokutana naye na kuishi naye kwa uwajibikaji mzuri, ushauri, ucheshi na kupenda mazoezi pamoja na michezo.

Kitu kingine kikubwa alichofanya wakati wa uhai wake, mbali ya kuinjilisha, alibadili mfumo wa kupokea



Padre JohnBosco Ndakimubuza

wanafunzi katika Shule ya Seminari ya Katoke, iliyopo Biharamulo, Kagera, ambapo wakati akiwa mwenyekiti wa bodi wa shule hiyo aliruhusu shule kupokea wanafunzi hata wasiokuwa na lengo la kusomea upadre.

Katika tanzia ya kifo chake Ndakimubuza, Askofu Severine Niwemugizi, wa Jimbo Katoliki la Rulenge-Ngara, kwa niaba ya Ndakimubuza, aliomba msamaha wote waliokosewa na Ndakimubuza wakati wa kipindi cha uhai wake hapa duniani.

Pambazuko tunawapeni pole wanafamilia wote, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Tunatoa pole kwa mapadre, watawa, na waumini wote katika jimbo la Rulenge-Ngara na majimbo mengine ambao msiba huu umewagusa kwa namna ya pekee.

### Tutakumbuka Daima...



*Kwamba Rais wa Kwanza wa Tanganyika huru na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alimpokea na kufanya mazungumzo na Malkia Elizabeth II wa Uingereza Jijini Dar es Salaam. Malkia huyo alikuwa Tanzania kwa ziara rasmi Julai, 1979. Malkia alifariki dunia Septemba 8, 2022. Mwalimu pia ni marehemu. (Picha kutoka mtandao wa intaneti)*

---

Njeo katika kitenzi



Na Dkt. Michael Mashauri

**K**ISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Lugha ya Kiswahili ina njeo (tenses) tatu: njeo iliyopo, njeo iliyopita na njeo ijayo. Njeo hizi hutambuliwa na viambishi mahsusi vinavyojitokeza katika kitenzi baada ya kiambishi kiima.

Leo tutajifunza jinsi njeo zinavyojitokeza katika kitenzi kwa mifano mbalimbali ya sentensi. (Kiswahili language has three tenses: present tense, past tense and future tense. These tenses are introduced by specific affixes in the verb after the subject concord. We will learn how these tenses appear in the verb through various sentences.)

A. Njeo iliyopo (Present tense)

Subject prefix	Present Tense	Root/stem	Examples
ni-	-na-	-soma	Mimi ninasoma sasa (I am reading now)
tu-		-kula	Sisi tunakula wali leo (We are eating rice today)
u-		-cheza	Wewe unacheza mpira (You are playing football)
m-		-imba	Nyinyi mnaimba (You all are singing)
a-		-endesha	Yeye anaendesha basi (He/she is driving a bus)
wa-		-kunywa	Wao wanakunywa maziwa (They are drinking milk)

B. Njeo iliyopita (Past tense)

Subject prefix	Past Tense	Root/stem	Examples
ni-	-li-	-pika	Mimi nilipika ugali (I cooked ugali)
tu-		-safiri	Sisi tulsafiri jana (We travelled yesterday)
u-		-ruka	Wewe uliruka jazi (You jumped the day before yesterday)
m-		-farahi	Nyinyi mlifarahi (You all were happy)
a-		-kuja	Yeye alikuja wiki iliyopita (He/she came last week)
wa-		-nawa	Wao walinawa mikono (They washed hands)

A. Njeo ijayo (Future tense)

Subject prefix	Future Tense	Root/stem	Examples
ni-	-ta-	-kaa	Mimi nitakaa chini (I will sit down)
tu-		-amka	Sisi tunaamka mapema sana (We will wake up very early)
u-		-tembea	Wewe utembea kwa miguu mwezi ujao (You will walk on foot next month)
m-		-oga	Nyinyi mtakimbia kesho (You all will run tomorrow)
a-		-kuja	Yeye atakuja wiki ijayo (He/she will come next week)
wa-		-fanya	Wao watafanya kazi keshokutwa (They will do work the day after tomorrow)

• Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.



### Malkia, ukoloni na utaifa

Na Pericles KALIMANGONGA

**M**ALKIA Elizabeth II wa Uingereza, amefariki dunia Septemba 8, 2022, akiwa na umri wa miaka 96. Alikuwa Malkia wa Uingereza kuanzia 1952. Utawala wake umedumu kwa miaka 70.

Elizabeth II alikuwa kiongozi wa taifa mojawapo, kati ya mataifa 14, yaliyoshiriki kwenye Mkutano wa Berlin uliogawanya Bara la Afrika katika mataifa 50, ambapo Uingereza ilipata kibali cha kutawala nchi 16 za Afrika.

Kwa sababu hii, kifo cha Elizabeth II kimesindikizwa na tanzia zilizoambatana na ukosoaji kutoka kwa Waafrika.

Tukumbuke kwamba, Mkutano wa Berlin ulikuwa ni mwendelezo wa sera za Wazungu kwa miaka 400 ya biashara ya watumwa kupitia bahari ya Atlantiki.

Katika biashara hii, Wazungu walikuwa wanawachukulia Waafrika kama bidhaa kwenye soko la biashara ya utumwa. Biashara hii ilimaliza sana nguvu za kimwili na kiakili za Waafrika na kuharibu msingi wao wa kiuchumi.

Kwa mujibu wa kitabu cha Walter Rodney; "How Europe Underdeveloped Africa (1972)," biashara hii iliambatana na ukandamizaji na unyonyaji wa Ulaya dhidi ya Afrika. Rodney anatoa ushahidi kuonyesha madhara ya kuviziwa, kutekwa, kusafirishwa na kuuzwa kwa Waafrika huko Ulaya na Amerika.

Wanunuzi wa watumwa kutoka Afrika walipenda watu wenye nguvu na afya bora, umri kati ya miaka 15 na 35, uwiano wa kijinsia ukiwa wanaume wengi zaidi kuliko wanawake. Hawakutaka wazee wala wenye ulemavu. Hata uchumi wa Afrika ulidumaa kwa sababu ya kuporwa kwa nguvukazi hii.

Biashara ya watumwa iliwapatia faida kubwa Wazungu. Lakini, biashara hii iliambatana na uporaji mkubwa wa rasilimali za Afrika.

Kwa mfano, sarafu ya Uingereza ya mwaka 1663 ilitwa "Sarafu ya Guinea"



Malkia Elizabeth II

kwa sababu ilitengenezwa kutokana na dhahabu kutoka Guinea Bissau, Afrika Magharibi.

Kwa sababu ya faida zilizotokana na biashara ya utumwa, bandari kubwa za ulaya zilizaliwa na kushamiri, zikiwemo Bristol, Liverpool, Nantes, Bordeaux na Seville.

Kwa upekee, Waingereza walifaidika zaidi na biashara ya utumwa. Kwa mfano, Rodney anaripoti kuwa, Benki za Barclays na Lloyds zilianzishwa miaka ya 1756 kwa kutumia faida iliyotokana na biashara ya utumwa.

Kwa hiyo, tunapoomboleza kifo cha Malikia Elizabeth II ni jambo muhimu kutafakari juu ya mema na mabaya ya Uingereza dhidi ya Afrika, kusudi tujifunze kutokana na historia yetu.

---

## ‘Tuepuke magonjwa ya akili’

Na Tryruckia MFINANGA

**H**IVI sasa habari kubwa zinazojaza kurasa za magazeti, muda mrefu kwenye redio na televisheni na kufurika kwenye mitandao ya jamii, ni zile zinazohusu wapenzi kuua ama kujeruhi.

Tatizo linakuwa kubwa kila uchao na wengi wenye imani za kidini wadai shetani, “ameongeza nguvu,” lakini kwa hakika ni kuwepo kwa ongezeko la magonjwa ya akili.

Wataalamu wa afya na madaktari bingwa wa magonjwa ya akili, wanakiri kwamba Tanzania imekuwa kinara wa matukio yenye dalili kwamba watu wanaokabiliwa na magonjwa ya akili wameongezeka.

Mabingwa wa magonjwa hayo wanaeleza kwamba magonjwa ya akili ni matatizo ya ubongo ambayo humfanya mtu kuwa na hisia, fikra na matendo tofauti na yale yanayotarajiwa na jamii na kushindwa kukabiliana na changamoto za maisha.

Kwamba magonjwa ya akili yanaweza kusababishwa na sababu mbalimbali ambazo wataalamu hao wanazigawanya katika makundi mawili; kibaiojia au kisaikolojia, huku msongo wa mawazo ukitajwa kujumuishwa.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linaeleza kwamba usaidizi wa kisaikolojia kwa watu waliokumbwa na kiwewe au msongo wa mawazo upatiwe umuhimu ili kupunguza madhara yatokanayo na ugonjwa huo.

WHO katika takwimu zake za hivi karibuni zaidi, inaonyesha kwamba duniani kote mtu mmoja kati ya watu 10 ni mgonjwa mtarajiwa wa magonjwa ya akili, hivyo kuzitaka serikali kutumia rasilimali kuelimisha na kutibu magonjwa hayo haraka.

Mtetezi wa haki za binadamu, Godlisten Malisa anaeleza kuwa hivi sasa habari za watu kujiua au kuua kwa sababu ya mapenzi au ugumu wa maisha ni kubwa nchini Tanzania na sababu



Mwenye msongo wa mawazo

kubwa ni kuwepo kwa ongezeko la matatizo ya akili.

“Kujiua kwa sababu ya matatizo ni kuwaachia matatizo makubwa zaidi uliowaacha, iwe mke na watoto au ndugu wa karibu kwani wanaenda kukabiliana na changamoto nyingi za maisha baada ya mtu kujiua, kuliko changamoto walizokua nazo kabla,” anaongeza.

Anasema, ikiwa mtu anaipeleka familia yake; mkewe, watoto, na ndugu, kamwe asijiue. Kujiua ni ubinafsi. Kujiua ni njia rahisi ya kumaliza matatizo yako, lakini kuacha matatizo makubwa zaidi kwa ndugu na marafiki. Na Kuongeza “kujiua ni kuacha alama ya maumivu isiyofutika kwa familia.”

Anashauri kwamba matatizo yakimzidi mtu, ni vyema akahakikisha anashirikisha watu wake wa karibu hata kama hawana uwezo wa kuyatatua – kwani kufanya hivyo, ni mwanzo wa kuepuka kuchukua uamuzi mbaaya.

### Montini: Sheria ya ndoa na uzazi

Na Deusedith KAHANGWA

**K**IFUNGU cha tisa cha sheria ya ndoa ya Tanzania (1971), kinafafanua maana ya ndoa. Kinasema kwamba, “ndoa ni muungano wa hiari wa mwanamume na mwanamke, unaokusudiwa kudumu kwa maisha ya pamoja yote.

Ufafanuzi huu wa kiuchambuzi kwa kutumia mapitio kadhaa ya kifalsafa, hauruhusu wananchi kusema nini hasa ni ndoa na nini siyo ndoa.

Makala haya yanaangalia zaidi mapitio kwa kuzingatia hoja za kifalsafa kama zilivyoandaliwa na Giovanni Battista Montini (1897-1978).

Montini alikuwa Mitaliano ambaye hakuwa na mke wala mtoto. Aliandika vitabu saba. Kitabu chake cha mwisho, “Maisha ya Binadamu” au “Humanæ Vitæ” kwa Kilatini, kiliandikwa mwaka wa 1968.

Hoja yake kuu katika kitabu hiki inawasilishwa kwa maneno 6,989 pekee ya Kiingereza. Kwa mujibu wa ibara za 8-9, 11, na 12-14 za kitabu hiki:

“Ndoa ni uhusiano kati ya mwanamume na mwanamke unaoanzia kwenye ahadi ya kuishi pamoja kama mke na mume na kukamilishwa na tendo la ngono ambalo ni: alama ya umoja, alama ya uzazi, alama ya utulivu wa kimwili na kiakili, lenye ubaguzi dhidi ya watu wote baki, na lenye uendelevu hadi kifo kinapowatenganisha wahusika.” (usanisi wangu).

Kwa akili ya Montini, ninavyoitafsiri, ufafanuzi huu unajumuisha hoja nane muhimu ambazo nitazifafanua kwa ufupi hapa chini.

**Moja**, ni “hoja kuhusu alama inayobeba maana ya uzazi,” ambayo ni kama ifuatavyo; sababu ni alama ya matokeo yake, kama ambavyo mawingu ni alama ya mvua hata kama mvua haitanyesha.

Kwa sababu ya kuruhusu manii na yai kukutana kwa ajili ya urutubisho,



Montini

ngono ya jenitalia kwa jenitalia wakati mwingine ni sababu ya uzazi.

Kwa hiyo, ngono ya jenitalia kwa jenitalia ni alama ya uzazi, kwa maana kwamba ngono ya jenitalia kwa jenitalia ni “alama inayobeba maana ya uzazi.”

**Mbili**, ni “hoja kuhusu alama inayobeba maana ya umoja,” ambayo ni kama ifuatavyo: Sababu ni alama ya matokeo yake, kama ambavyo hasira ni alama ya ugomvi hata kama ugomvi hautatokea.

Kwa sababu ya homoni ambayo ni kiunganishi cha kimahaba (oxytocin), ambayo uzalishaji wake huchochewa na ngono, ngono ya jenitalia kwa jenitalia wakati mwingine ni sababu ya umoja kati ya watu.

Kwa hiyo, ngono ya jenitalia kwa jenitalia ni alama ya umoja, kwa maana kwamba ngono ya jenitalia kwa jenitalia ni “alama inayobeba maana ya umoja.”

**Tatu**, ni “hoja kuhusu alama inayobeba maana ya utulivu wa kimwili na kiakili,” ambayo ni kama ifuatavyo: Sababu ni alama ya matokeo yake, kama ambavyo mawingu ni alama ya mvua hata kama mvua isiponyesha.

*Itaendeela wiki ijayo...*

---

## Upendo na sauti inayokita anga

Na Shabaan LULELA

**Y**AWEZEKANA Upendo Manase ni jina geni kwa Watanzania wengi, lakini ni kubwa kwa wapenzi wa muziki wenye vionjo vya Afrika – hasa kusini mwa jangwa la Sahara.

Muziki wa Upendo umeenea zaidi Ujerumani, Uswidi, Denmark, Kenya, Uganda, Ufini na maeneo mengine ambako hualikwa mara kwa mara kwa ajili ya matamasha.

Wapenzi wengi wa muziki kwa kusikiliza nyimbo za Upendo, wanakiri kwamba mwanamuziki huyo wa Tanzania ni chapa ya galasa la muziki duniani, akitokea Afrika Kusini, Miriam Makeba.

Sifa za Miriam Makeba, pamoja na kwamba sasa ni marehemu, ni kubwa na zinaendelea kuweka sifa za uzuri wa nyimbo na ala za muziki wa Afrika.

Wengi wanaomsikiliza Upendo akiimba; iwe mubashara au kupitia redio na televisheni, wanaeleza kuwepo kwa shabahi ya mpangilio wa sauti ya Makeba ndani na mwanamuziki huyo asiyevuma sana Tanzania.

Waliomsikia kwa mara ya kwanza Upendo akitumbuiza kwenye tamasha kubwa la muziki Zanzibar, Sauti za Busara mwaka huu, 2022 watakuwabaliana na wale wanaoeleza kuwa Miriam Makeba, amepata mwanamama anayejaribu kuvaa viatu vyake, ingawa ukweli unabaki pale pale kuwa nguli huyo wa muziki kutoka Afrika Kusini nafasi yake haiwezi kuzibwa. Makeba atabaki Makeba!

Upendo aliyeanza kuimba kanisani tangu akiwa binti mdogo jijini Dar es Salaam, hivi sasa ana albam moja yenye nyimbo nane ikiitwa – Wake Up (ikiwa na tafiri ya “Amka” kwa Kiswahili).

Katika albam hiyo yenye nyimbo zenye vionjo vya mitindo ya Afropop, ala za kienyeji na marimba, Upendo ameimba kuhusu maisha ya kawaida ya Watanzania wengi, hasa wanaoishi vijijini, hali ya kisiasa, ubaya wa ukoloni katika lugha ya picha na uhusiano wa watu.



Upendo Manase

Upendo ambaye pia ni mwalimu wa sauti katika Chuo cha Muziki cha Action, kilichopo Mbezi, Dar es Salaam, anasema pamoja na kupenda nyimbo zenye mtiririko wa sauti na vyombo vinavyoendana na mitindo mingi ya uimbaji wa asili, anapenda zaidi mchanganyiko wa mapigo ya ala za Kiafrika na muziki wa kisasa hasa kutoka Bara Hindi na Karibeani.

Matamano ya Upendo ni kuutangaza zaidi ‘muziki wa Tanzania’ ambao anaamini ni mzuri zaidi, ingawa nchi bado haijautambua na kuipaisha.

# PICHA KUBWA



Wanyama wanapokutana ni raha iliyoje. Hapa ni mbuga ya wanyama ya Ethosha iliyoko Namibia, ni maarufu kwa kuwa na wanyama anuai kama iliyo kwa Serengeti na Ngorongoro zinazopatikana Tanzania. Picha hii ilipigwa na Doug Poole na kutumiwa kwa mara ya kwanza na gazeti la Daily Marverick.

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

